Upande wa utetezi yaani New Africa Hotel Ltd. ulileta mashahidi wawili yaani Bwana Manongi Kilembe na Bwana John Lotuma. Bw. Manongi aliiambia Mahakama ya kuwa aliwahi kuajiriwa na Hotel New Africa kama Mkurugenzi wa Ndani, mwaka 1995 hadi sasa. Bw. Manongi alielezea utaratibu wa kazi zilizokuwa kwa Receptionist kuwa walipokezana. Alisema kila Receptionist aliyemaliza zamu yake alifunga pesa za makusanyo kwenye Banking Bag na kuzikabidhi kwa meneja wa zamu DW. 1 alitoa kitabu cha Hotel procedure kielelezo D.1 alisema kuwa baada ya Bw. Marwaha kulipa mara mbili. Bi Agnes alifanya masahihisho na kuonyesha mgeni amelipa entry moja tu. DW. 1 alisema kuwa Bi Agnes hata baada ya kufanya correction hakuarifu menejiment. DW. 1 alieleza mahakama kuwa menejiment ilijua juu ya "double posting" baada ya Bw. Marwaha kupiga simu na kusema kuwa alilipa mara mbili Bw. Manongi alitoa Bill ya terehe 17/11/98 iliyopokelewa kielelezo D.3 na pia barua ya Elizabeth iliyopokelewa kielelezo D.2. Shahidi wa pili upande wa utetezi Bw. John Lotuma (D.2) aliyeajiriwa kama Human Resources Manager alisema alifahamu Mlalamikaji Bi. Agnes na alitoa barua ya ajira ya Agnes Mlalamikaji Exht

D.5. Alieleza kuwa Mlalamikaji aliachishwa kazi kwa kutofuata taratibu za kuchukua fedha kwa mteja. DW. 2 alimalizia kwa kusema kuwa hatua hizo zilianza baada ya mteja kulalamika. Hata hivyo kwa hatua hizo shahidi alielezea kuwa mlalamikaji alipewa haki zake zote na hazikukanushwa na mlalamikaji pia.

Katika kujibu hoja za wakili wa mlalamikaji, shahidi wa pili alisema kuwa mlalamikaji hakutakiwa kukaa na fedha za mteja na kwamba Mlalamikaji alizirudisha baada ya mteja kulalamika. DW. 2 alielezea mahakama hii kuwa kwa mlalamikaji ilikuwa kosa lake la kwanza na waliamua kumpunguza kazi. Huu ulikuwa mwisho wa ushahidi kwa upande wa Walalamikaji/utetezi na pia upande wa mlalamikaji.

Kamishna wa kazi alipoleta mgogoro huu kwa uchunguzi chini ya kifungu cha 8(a) cha Sheria ya Mahakama ya Kazi Na. 41 ya mwaka, 1967 kama ilivyorekebisha na Sheria Na. 2 ya mwaka, 1993 alitaka Mahakama hii ichunguze mambo yafuatayo na kuyatolea uamuzi.

- (1) Kama taratibu za kumwachisha kazi mfanyakazi huyo zilizingatiwa kisheria.
- (2) Kama sababu za kumwachisha kazi zilitokana na mfanyakazi huyo kukiuka taratibu za hoteli zinahusu namna ya kuhifadhi fedha za mteja.
- (3) Kama mahusiano Kati ya Meneja Mkuu na Mlalamikaji ndio chanzo cha mgogoro.
- (4) Kama Mlalamikaji alipewa nafasi ya kujieleza kaba ya kuchukuliwa hatua.
- (5) Kama kuchukua haki zake kunaweza kumzuia mfanyakazi huyo kutoendelea kulalamika hatua ya kiachishwa kazi.
- (6) Masuala mengine yeyote ambayo mahakama itaona yanafaa kuchunguzwa kwa madhumuni ya kuiwezesha mahakama yakazi kufikia uamuzi wa haki na Tuzo.

Nikizipitia "final submissions" zilizowasilishwa na pande zote mbili zilizoandikwa kwa lugha ya kiingereza upande wa mlalamikaji nikitumia lugha ya mahakama hii Kiswahili ninasema kuwa utaratibu wa kumwachisha kazi mfanyakazi wake haukufuatwa. Msomi Ami anasema kuwa upande wa mwajiri ulifuata taratibu zilizoweka na "Staff Book" ambao mwajiri alisema kuwa mfanyakazi alikubaliana na taratibu hizo kwa hiari yake alipoajiriwa.

Msomi Ami alikataa kitendo cha mwajiri cha kutumia "Staff Book" kumwajibisha mfanyakazi. Alisema huko ni kukiuka taratibu zilizowekwa na sheria kutumika na mwajiri alitakiwa afuate taratibu zilizowekwa chini ya Sheria ya Usalama Kazini (Security of Employment Act) na si "Staff Book". Alisema mwajiri alitumia hujia fupi ya kumkomoa mwajiriwa na hivyo kupingana na "Security of Employment Act".

Akiendelea na hoja za mwishi Msomi Ami alieleza kuwa kitendo cha "double posting" kilisababishwa na meneja Bw. Manish, akaendelea kueleza kuwa haikuwa kazi ya Bw. Manish bali ni kazi za Cashier (mweka Hazina) hivyo haikuwa sahihi kumwajibisha Cashier kwa kosa lililofanywa na Manager

ambaye hakumwarifu Cashier kuwa ameshapost fedha za mteja.

Akajadili kitendo cha kuweka fedha kwenye locker, Msomi Ami alisema kuwa haoni kosa la mteja wake kuhifadhi fedha za mteja wa Hotel Mr. Marwaha katika Locker alizitoa zilipotakiwa. Alisema kuwa kitendo hicho kilipaswa kumpelekea mwajiri kupata onyo na si kuachishwa kazi. Ami alisema kwa niaba ya mteja wake Agnes aliripoti kwa Elizabeth ambaye alikuwa ni Supervisor wake kwa hiyo hakupaswa kuachishwa kazi kwa kitendo hicho cha kwanza.

Katika maelezo ya mwisho Msomi Ami aligusia sababu za uzee kuwa ndiyo iliyosababishwa mteja wake kuachishwa kazi. Kwa vile ushahidi huo au aliyesikia hakuja kuihakikisha mahakama juu ya jambo hili naona haya ni maneno tu ya kusikia (hearsay evidence). Msomi Mr. Ami hakuwa na la kupinga kuhusu kupewa nafasi ya kujitetea.

Akijibu hoja ya tano alitoa kesi mbili ya MOHAMA VS THE UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM (1981) T.L.R. na ALLY LINUS & 11 OTHERS VS TANZANIA HARBOUS AUTHORITY and another Civil Appeal No 2 of 1983, Court of Appeal of Tanzania (unreported) zilizojadiliwa kuhusu kudanganyika kuchukua mafao baada ya kuachishwa kazi. Msomi Ami alisema kuwa waajiri walizoea kuwadanganya kuchukua mafao ili wasiwe na nafasi ya kuleta madai dhidi ya mwajiri.

Kwa kumalizia Msomi Ami alisema kuwa kuachishwa kazi kwa mlalamikaji kulikuwa rahisi kwa kukosekana Tawi la Chama mahala pa kazi. Alisema kuwa lingekuwapo tawi la chama isingelikuwa rahisi kwa mwajiri kutoa adhabu ya kumwachisha kazi mfanyakazi.

Kwa hitimisho Msomi Ami alisema kuwa kutokuwepo Tawi la Chama cha Wafanyakazi mahali pa kazi kunakuwa ni kukiukwa taratibu na kuwanyima haki za kikatiba (constitutional right) Mahakama ya Kazi. Hivyo aliomba mahakama hii imwamuru mwajiri amrejeshe kazini mfanyakazi.

Kwa upande wa mwajiri katika hoja za mwisho (final submission) ziliwasilishwa na Msomi Wakili Fatma. alikubaliana kuwa kifungu cha 37 (1) (b) cha Sheria ya Usalama Kazini kinatoa utaratibu wa kufuata wakati mwajiri anamwachisha kazi mfanyakazi, na akasema kuwa katika kesi mwajiri alifuata taratibu zote zilizowekwa na sheria iliyotajwa hapo juu na kumalizia kwa kusema kuwa mfanyakazi alipoajiriwa alikubali masharti yote kwa hiari yake. Pia alizungumzia nidhamu kwa wafanyakazi ili kuvutia wateja. Alisema bila nidhamu wateja wangelikimbia hoteli. Msomi Fatma alisema kuwa kitendo cha mfanyakazi alichokitenda na mwajiri kumwachisha kazi kilikuwa sahihi ili kuwadhibiti wafanyakazi.

Katika kujibu hoja ya pili Msomi Fatma alisema "double posting" haikusababishwa na Manager bali ilisababishwa na mfanyakazi na ndiyo maana aliomba radhi. Alisema kama hakufanya kosa kwa nini aliomba radhi? Pia alisema kitendo cha Manager kupost Bill ya Customer ni cha kawaida kwani

kingeliweza kujionyesha kwenye computer na hivyo kumfanya Agness asiingize tena mara ya pili.

Akielezea zaidi Msomi Fatma alisema kuwa kama hiyo haikutosha, mfanyakazi Agness alifanya (correction) masahihisho na kuchukua pesa za mteja na kuzihifadhi kwenye locker. Msomi Wakili Fatma alisema kuwa Lockers zilitumika kuhifadhi nguo zao, wanapokuwa kazini na siyo pa kuhifadhi fedha. Hivyo Msomi Fatma akasema kuwa mfanyakazi alikiuka taratibu za kuhifadhi fedha za wateja.

Akijibu hoja za maandishi za mlalamikaji Fatma alisema kuwa Mlalamikaji hakudanganywa ili apokee mafao yake kwa kumziba mdomo asilalamike. Fatma alisema kuwa Mlalamikaji alivunja masharti ya mikataba ya ajira na hivyo kulipwa mafao yake kama yanavyotakikana na sheria.

Msomi Fatma alikubali kuwa hili lilikuwa kosa la kwanza kwa mlalamikaji na akasema walimwachisha kazi kuzuia vitendo hivyo visiendelee kwenye hoteli. Na kupinga zaidi suala la mlalamikaji kurudishwa kazini kwani alisema kuwa ingeliwapa kichwa ma-cashier wengine watakaofanya vitendo kama hivyo.

Msomi Fatma alidai kuwa taratibu hazikufuatwa hadi kuleta shauri hili mahakamani. Kwani amedai kuwa Afisa wa kazi hakukubali kuachisha suluhisho mwajiri alipokuwa na shida na badala yake akalipeleka shauri hili kwa Kamishana wa Kazi. Aliendelea kueleza kuwa Afisa wa Kazi alitakiwa ajitahidi kusuluhisha ili kufikia mwafaka badala yake akaliharakisha kupeleka kwa Kamishana wa Kazi.

Akihitimisha aliomba rai kwa mahakama hii kutokubali kumrejesha mlalamikaji kazini na hivyo kuomba madai ya mlalamikaji yatupiliwe mbali.

Nikianzia na hoja ya kwanza, kwa vile hakuna tawi la Chama cha Wafanyakazi mahala pa kazi hivyo inaonyesha kuwa management ilimwandikia barua ya kujieleza tu. Vile vile mlalamikaji alitakiwa na Bw. Nick kuomba radhi na kurudisha fedha za mteja. Tukuangalia sheria inasemaje kifungu cha 37 cha Sheria ya Usalama kazini kinamtaka mwajiri anapokusudia kumwachisha kazi mfanyakazi impe notisi ya mwezi. Tukuangalia kwa upande wa Mlalamikaji baada ya kuzirudisha fedha za mteja, Meneja Bw. Manish alimwandikia kimemo na kumpa barua ya kumwachisha kazi. Zaidi ya kimemo hakuna notice aliyompa ikihusu kusudio la kumwachisha kazi. Ingawa upande wa mlalamikaji ulidai kuwa taratibu za kumwachisha kazi mfanyakazi zilifuatwa kisheria lakini Msomi Wakili wa Mlalamikaji hakusema ni sheria zipi zilifuatwa. Alichokieleza ni kuwa mfanyakazi alikubali masharti ya ajira kwa hiari yake. Je, kukubali masharti ya ajira ndiyo aachishwe kazi bila kufuata sheria inayoongoza masuala ya ajira.

Katika kujibu suala hili sina budi kueleza kuwa mikataba yote ya ajira inaongozwa na Sheria ya Kazi (Employment Ordinance) na Sheria ya Usalama Kazini (Security of Employment Act). Sheria hizi zimetungwa na Bunge ili kulinda wafanyakazi na mwajiri kwa ujumla.

Sheria hizi hazina budi kufuatwa katika kulinda haki za mwajiri na mfanyakazi. Pindi zinapokiu kwa basi anayehusika itakuwa amenyimwa haki za msingi.

Kipengere cha pili ni kama sababu za kumwachisha kazi zilizotokana na mfanyakazi huyo kukiuka taratibu za hoteli zinazohusu namna ya kuhifadhi fedha za mteja. Katika ushahidi uliotolewa na John DW.2 alisema kuwa fedha hizo (PW. 1) Agness aliziweka fedha hizo kwenye kabati la kuhifadhi nguo zao za kazi.

Vile vile kuna ushahidi kuwa Bw. Manish alifanya Posting ya kwanza. Suala la kujiuliza kwa nini Agness hakumwarifu Manager baada ya kugundua hiyo double posting? Ushahidi uliotolewa na pia maelezo ya Elizabeth Kirima yalieza kuwa nanukuu "Agness aliripoti kwamba mgeni Mr. Marwaha ana over charge ya Bill yake ndipo nilipoamua kama Shift Leader kumruhusu Agness kuhifadhi pesa hiyo kwenye Safe ili akija arudishiwe.

Hakuna ubishi kuwa hata kwenye ushahidi kuwa Agness alipotakiwa kutoa fedha hizo alizitoa zote. Suala la kuwa na pesa hizo zilitolewa kwenye nini sidhani kama ni suala la msingi. Kwani pesa hizo zilitolewa kwenye kabati, tena kabati la Agness la kuhifadhi nguo. Pia tukirudi nyuma ni kuwa mgeni Mr. Marwaha alichek out tarehe 18 Novemba, 98. Na katika barua zake pia Bi. Agness alikubali kuwa aliweka fedha hizo kwa vile aliamini kuwa Bw. Marwaha atakuja kwa vile yeye ni mteja wao mara kwa mara. Nanukuu memo ya Bi. Agness ya tarehe 22/12/98

Exht 1.

" I kept the cash in my locker not for sealing but because Mr. Marwaha is our regular guest and cash was to be handed over as soon as he check in".

Kama Agness asingelikuwa mwaminifu, asingelitunza fedha hizo zilizosababishwa na kuingiliwa na meneja aliyekiingiza kwenye kazi za receptionist. Na kwa kufanya hivyo, Mlalamikaji amebeba mzigo mzito wa kuachishwa kazi wakati meneja akifurahia na kuendelea na kazi. Katika uchunguzi huu nimeona kuwa taratibu hazikufuatwa na pia kulikuwa ni kama uonevu. Pia katika ushahidi umeonyesha kuwa mlalamikaji hajawahi hata kufanya kosa lingine wala kuonywa kwa kosa lolote lile.

Tatu kama mahusiano kati ya Meneja Mkuu na Mlalamikaji ndiyo chanzo cha mgogoro. Hakuna ushahidi uliotolewa na upande wowote unaoonyesha kuwa kulikuwa na aina fulani ya mahusiano kati ya watu hawa wawili. Katika hoja za mwisho zilizowasilishwa na msomi Wakili Ami alimtetea Mlalamikaji aligusia kuwa mteja wake alisikia toka kwa rafiki yake wakisema mlalamikaji kuwa mzee. Hii napenda kumfahamisha Msomi Wakili Bw. Ami kuwa mahakama mara nyingi haitilii maanani ushahidi wa kusikia (hearsay) hasa ukizingatia kuwa hata huyo aliyesikia hakufika kuja kutoa ushahidi. Hivyo kwa upande wa mahakama (with due respect) hoja hiyo haina msingi.

Nne kama Mlalamikaji alipewa nafasi ya kujieleza kabla ya kuchukuliwa hatua. Katika kuchunguza hatua hiyo mlalamikaji aliandika barua "D.4" ya tarehe 2/12/98 alijibu "memo" ya Manish kwa tuhuma hizo na kwa majibu hayo alitakiwa ajieleze. Kwa vile hiyo "memo" haikutolewa mahakamani, imekuwa ni vigumu kujua malalamiko au shutuma alizotakiwa kujibu ni zipi.

Tano kama kuchukua haki zake kunaweza kumzuia mfanyakazi huyo kutoendelea kulalalmika hatua ya kuachishwa kazi. Katika kuchunguza shauri hili hakuna kitu chochote wala sheria yoyote inayokataza mlalamikaji kuchukua mafao yake na asilalamikie hatua ya kuachishwa kazi. Mlalamikaji katika shauri hili analalamika kuwa kuachishwa kwake kazi hakukuwa halali. Yeye hakulalamikia malipo. Hata akilalamika kuhusu malipo hakatazwi na sheria kutochukua anacholipwa kwanza.

Baada ya kuchambua hoja zote ambazo Kamishna wa Kazi aliitaka mahakama hii kuzifanyia uchunguzi, mahakama iliwapa nafasi washauri wote kuleta maoni yao. Washauri hao hawakuweza kuniletea maoni yao mpaka wakati naandika uamuzi huu.

Kama nilivyokwisha chambua ushahidi na mambo ambayo Kamishna wa Kazi aliyetaka tuyachunguze mambo yafuatayo nimeona kuwa la kwanza nimeridhika kuwa taratibu zilifuatwa na mlalamikaji zinazotakikana na sheria ila kwa upande wa mwajiri hakufuata taratibu zinazotakiwa katika kumwachisha kazi, kwani alitakiwa aweke kikao na yajadiliwe mbele ya kikao. Nimeridhika kuwa mwajiri alikiuka taratibu zilizowekwa na sheria kufuata na kuufanya utaratibu mzima kuwa batili. Katika kuchunguza hoja ya pili nimeridhika kuwa Hoteli ya New Africa hawakuwa na mwongozo mzuri wa kuwadhibiti wafanyakazi. Kila mmoja alijifanyia kazi kiholela bila kufuata taratibu zilizowekwa na sheria. Kufuata mwenendo uliowekwa wa "Staff Book" huo ulikuwa ni mwongozo tu uliowekwa na hoteli na siyo sheria. Pia yeye mwajiri hakuwa na utaratibu mzuri juu ya fedha za wateja zilizolipwa ziada. Kama hayo yalitokea pia kwa wengine na kama walivyosema kwenye ushahidi wao kuwa siyo mara ya kwanza mteja kuzidisha fedha, hakuna adhabu yeyote waliyoitoa kwa wenzake. Hivyo naamini kuwa kuachishwa kazi mlalamikaji kulikuwa kwa uonevu na bila kufuata taratibu zilizowekwa na sheria.

Vile vile nikizingatia hoja ya tatu ni wazi kuwa mlalamikaji alinyimwa haki yake ya msingi kusikilizwa. Badala yake kupewa adhabu ya kuachishwa kazi hivyo kukiuka misingi yote iliyowekwa na sheria.

Kufuatia yote hayo na sababu nilizozitoa hapo juu naamini na kwa kufuata sheria ya usalama kazini na sheria za kazi utaratibu mzima wa kumwachisha kazi mlalamikaji haukufuatwa na hivyo kulifanya zoezi zima kuwa batili.

Kwa hiyo basi naamuru mlalamikaji arejeshwe kazini mara moja. Alipwe haki zake zote toka tarehe aliyoachishwa kazi Januari, 1999, hadi tarehe ya uamuzi huu.

CT: Baada ya kumaliza kuandika na kabla ya kuusoma uamuzi huu; muungwana mshauri Bw. Mjema alileta maoni yake saa 5.20 asubuhi wakati nimewaeleza wahusika kuwa uamuzi nitausoma saa 8 mchana.

Hivyo naandika maoni yake kama alivyoandika kuwa:

Bi Agness Nyongole, hakutendewa haki katika kuachishwa kazi. Pia Bi Agness alipokea haki zake ili kumfanya aweze kuhimili maisha huku akiendelea na shauri lake. Vile vile aliandika kuwa Mlalamikaji hakukiuka taratibu zozote isipokuwa aligundua kosa la mkuu wake na hicho ndicho kitu kilichofanya aachishwe kazi. Mwisho alisema Mlalamikaji hakusikilizwa na kuhojiana ana kwa ana na wahusika wote katika shauri hili. Hivyo alitoa maoni kuwa Mlalamikaji arejeshwe kazini tangu tarehe ya kuachishwa kazi 6 Januari 1999.

Baada ya hapo sioni sababu ya kuyajadili maoni haya hapa kwa wakati huu, Washauri wanapaswa kuleta maoni yao mapema ili kuiwezesha mahakama kuyajadili kwa wakati muafaka, na siyo wanavyotaka wao. Hii inasabisha ucheleweshaji wa mashauri na kutowatendea haki wahusika.

Uamuzi huu umesomwa hapa Dar es Salaam tarehe 20/7/2001 mbele ya Bw. Kilembe (Internal Auditor wa New Africa Hotel).

(Sgd)
C. E. R. WILLIAM
Naibu Mwenyekiti

20/7/2001

Certified true copy of the original.

01 Agosti, 2001,

B. E. NYAMUBI,
Registrar

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 129

UCHUNGUZI WA MGOGORO WA KIKAZI

NA. 37 WA 1999

baina ya

ND. NDOWO JOSEPH, DAR ES SALAAM

na

SCANIA (T) LTD., DAR ES SALAAM

UAMUZI

WILLIAM, DC

Huu ni uamuzi unaotokana na uchunguzi wa mgogoro kati ya Bibi Ndowo Joseph na Scania (T) Ltd. Mlalamikaji

alianza kazi mwaka 1978 kama "Cadet Clerk". Baada ya kuhudhuria mafunzo ya Computer kielelezo P.1 kinavyoonyesha mlalamikaji alibadilishiwa kazi mwaka 1987 na kuwa Computer Operator, mwaka 1997 alipata nafasi ya masomo ya "Telephone Operator" na alipata cheti P.2.

Katika utendaji wake wa kazi mwaka 1985 alichaguliwa kuwa mfanyakazi bora kama ilivyo kwenye kielelezo P.3. Ilipofika tarehe 18.5.98 alipewa barua ya kupunguzwa kazi. Mlalamikaji hakuridhika na hatua hiyo na kudai kuwa Walalamikaji walikiuka masharti yaliyowekwa na kifungu cha 7 (saba) cha mkataba wa hiari. Mlalamikaji alitoa Mkataba wa hiari kielelezo P.5.

Akifafanua kuhusu kifungu hicho cha saba Mlalamikaji alidai kuwa kifungu kilisema wajumbe washirikishwe katika kujadili mkataba wa hiari, akasema kwa vile wajumbe hawakushirikishwa basi mkataba ulikuwa batili na hivyo kufanya upunguzwaji pia kuwa batili.

Jambo la pili, mlalamikaji alidai kuwa mwajiri alimpunguza kazi kabla ya mkataba kusajiliwa. Alisema kuwa alipunguzwa kazi mwezi wa tano (5) na mkataba kusajiliwa mwezi 11/98. Katika hoja ya tatu mlalamikaji anaeleza kuwa mwajiri aliajiri mtu mwingine aitwaye Magreth Chagula muda mfupi tu baada ya kumpunguza kazi kama alivyotoa kielelezo P.6. Mlalamikaji anadai kuwa alipotoka mafunzo ya Telephone Operator alikuta mtu mwingine akifanyakazi kama Telephone Operator/Receptionist na hivyo kukiuka masharti ya FILO.

Mlalamikaji aliitaka mahakama ipitie kesi ya JUMUIYA YA WAFANYAKAZI DHIDI YA MOROGORO REGION COOPERATIVE 6/92 alisema mahakama hii ilisisitiza masharti ya FILO yafuatwe.

Jambo la nne Mlalamikaji anadai kuwa alistahili pia kulipwa mafao ya kutimiza miaka 100 ya kampuni akadai kuwa mwajiri hakumlipa kwa madai kuwa waliostahili ni wafanyakazi waliostaafu tu, kama alivyotoa kielelezo P.7.

Kutokana na hayo yote mlalamikaji aliiomba mahakama hii imwamuru mwajiri amrejeshe kazini.

Shahidi wa pili wa mlalamikaji (PW.2) Martin Yamo akiwa mfanyakazi pia wa Scania (T) Ltd. alisema kupunguza wafanyakazi kulifanyika ili kupunguza gharama za uendeshaji na pia kuondoa nafasi zisizo za lazima Bw. Martin alisema kuwa Scania iliondoa kwa kuwapunguza wafanyakazi wote wa Idara ya Ulinzi na kuleta askari wa kukodi. PW. 2 Martin alisema kuwa wafanyakazi wengine walipunguzwa ikiwa ni pamoja na mlalamikaji aliyekuwa Telephone Operator. PW.2 Martin alikubali kuwa Scania/ mwajiri hakutumia utaratibu sahihi wa kupunguza wafanyakazi. Alisema kuwa menejimenti waliwaita na kuwaeleza uamuzi wa mwajiri. PW.2 alisema kuwa ilitakiwa menejiment ikae na Chama cha Wafanyakazi ili kujadili masuala ya upunguzaji wafanyakazi na gharama

itapunguzwa vipi na wapi na siyo kujipangia tu na kuleta kwa utekelezaji.

PW.2 Bw. Martin alikiri katika ushahidi wake kuwa nafasi ya Ndowo imepata mwajiriwa mwingine baada ya yeye kupunguzwa kazi. Kwa hiyo alisema hakuna gharama yoyote liyopunguzwa kwa kumpunguza Ndowo.

Pia Bw. Martin alisema kuwa pamoja na kukubaliana na zoezi hilo lakini alisema kuwa taratibu zilikiukwa. Katika kujibu hoja ya menejiment, Bw. Martin alisema kuwa menejiment ilileta kwenye kikao waliyokwishayapanga ayari, hivyo hakuna walichojadili mwajiri na viongozi wa wafanyakazi. Na pia alisema kuwa wao walikubali kusaini ambayo ni makosa waliyoyafanya.

Huu ulikuwa mwisho wa upande wa mlalamikaji.

Akijibu hoja za mlalamikaji, Bibi Sharbano Kabisa ambaye ni Meneja Utawala wa Scania alisema kuwa taratibu zote zilifanyika katika kuwapunguza kazi wafanyakazi. Pia katika maelezo yake alisema kuwa waliwahusisha wahusika wote wa TUICO katika kujadili suala zima la kuwapunguza kazi kama ilivyoonyesha kielelezo D.1.

Bibi Kabisa alisema baada ya kikao cha kwanza, walikaa tena kikao kati ya TUICO na menejiment kama ilivyo kwenye kielelezo D.2 ya tarehe 21/4/98.

Bibi Kabisa alisema kuwa taratibu zote za kumwachisha kazi B. Ndowo zilifuatwa na kwa kusaini mkataba halali kati ya Scania na TUICO. Bibi Kabisa alikataa kwa kuajiri mtu mwingine badala ya Ndowo na kuiomba mahakama hii itupilie mbali madai ya mlalamikaji.

Kamishna wa Kazi alipouleta mgogoro huu kwa barua yake yenye Kumb. Na. KZ/U.10/MG/1138/4 ya tarehe 31/8/99 chini ya kifungu cha 8(a) cha sheria Na. 2/1993 aliiomba mahakama hii iyachunguze yafuatayo:—

- (i) Kama, Mkataba uliotumika kumpunguza kazi mlalamikaji ulikuwa halali.
- (ii) Kama ulikuwa na sababu yoyote ya msingi ya kumpunguza kazi.
- (iii) Kama katika nafasi yake aliajiriwa mtu mwingine
- (iv) Kama, utendaji wake kazi ulikuwa mbaya.
- (v) Masuala mengine ya kisheria ambayo yataiwezesha mahakama kutoa uamuzi na TUZO.

Baada ya kupata muhtasari wa ushahidi toka pande zote mbili walalamikaji na walalamikiwa suala la kwanza ambalo linapaswa kujadiliwa na kuamuliwa ni je ni kweli mkataba uliotumika kupunguza kazi mlalamikaji ulikuwa halali.

Nilipata maoni ya mshauri Bw. Pazi OTTU na sikupata maoni ya mshauri Bw. Kingazi, ATE. Hivyo mshauri Bw. Pazi nami tumeona ya kuwa lalamiko hili si la kweli hata kidogo. Upande wa Walalamikiwa umethibitisha ya kwamba Tawi la OTTU/TUICO la Kampuni ya Scania (T) Ltd. lilishirikishwa kikamilifu katika suala zima la kupunguza wafanyakazi wa kampuni hiyo. Kwanza kabisa Walalamikiwa

walitoa kumbukumbu za kikao cha pamoja kati ya uongozi wa kampuni ya OTTU/TUICO kilichofanyika tarehe 21/4/1998. Muhtasari huo uliotolewa na kupokelewa hapa mahakamani kama kielelezo D.1. Bw. M. Yamo shahidi wa pili (PW.2) alihudhuria kikao hicho kama Mwenyekiti wa Tawi la OTTU/TUICO. Agenda kuu ya mkutano huo ilikuwa nanukuu "kufuatia ufanisi duni wa kibiashara wa kampuni ya Scania Tanzania Branch kulikuwa na hoja ya kupunguza baadhi ya wafanyakazi" na kuwa kikao kilisema kuwa pande zote mbili zilikubaliana kwa hiari kama ilivyo kwenye mkataba wa hiari kati ya OTTU/TUICO na menejiment ya Scania Tanzania Branch 16/11/98. Mkataba huo ulifuata taratibu zote za utendaji zilizofuata misingi ya sheria.

Suala la kusema kuwa mkataba ulisajiliwa baada ya yeye kupunguzwa kazi halina msingi wowote kwani ungelirudishwa bila kusajiliwa hapo angelikuwa na sababu ya kuukataa mkataba.

Suala la pili ni je kulikuwa na sababu yoyote ya msingi ya kumpunguza kazi katika kulichunguza suala hili sehemu yake ya kazi ilikuwepo kwenye kigezo 1(b) katika mkataba wa hiari kuwa nanukuu

"(b) kufutwa kwa nafasi — baada ya kuwa na muundo mpya katika kampuni.

Mshauri Bw. Pazi nami tumeona ya kuwa ni kweli kwenye nafasi ya mapokezi ambayo ni nafasi aliyoajiriwa na kupunguzwa hapana mtu aliyeajiriwa badala yake. Ni kweli mlalamikaji wakati akipunguzwa kazi alikuwa Receptionist cheo hicho alikipata tarehe 3/2/1997.

Pia ni kweli mlalamikaji alihudhuria mafunzo ya Telephone Operator, lakini alishindwa kuleta kielelezo cha kuonyesha kuwa alibadilishwa toka Receptionist kuwa Telephone Operator. Kwa mtazamo wa kawaida kazi hizi mbili ziko tofauti ingawa zinaweza kufanywa na mtu mmoja. Barua ya Bi. Magreth Chagula aliyoleta ya tarehe 4/11/98 aliajiriwa kwa mkataba wa mwaka (1) kama Telephone Operator. Ndowo alipunguzwa kazi tarehe 31/5/98 hivyo ni miezi sita (6) baadaye. Margreth hakuajiriwa kama Receptionist.

Kwa hiyo pamoja na hayo yote tuliyosema hapo juu ni wazi kabisa kulikuwa na sababu za msingi za kumpunguza kazi mlalamikaji.

Jambo la tatu linalotakiwa kujadiliwa na kuamuliwa ni je utendaji wake wa kazi ulikuwaje.

Katika kujadili suala hili mshauri Bw. Pazi nami tumeona kuwa utendaji wake wa kazi mlalamikaji ulikuwa mzuri. Mlalamikaji aliwahi kuzawadiwa zawadi ya cheti cha mfanyakazi bora wakati wa sherehe mojawapo za wafanyakazi ulimwenguni kielelezo P.3.

Jambo la mwisho la kujadili kama masuala mengine ya kisheria ambayo yataiwezesha mahakama kutoa uamuzi na

TUZO. Katika kujadili suala hili zima na nikiungana na maoni ya ushauri wa muungwana **Bw. Pazi** tumelichunguza na kuona kuwa utaratibu mzima haukufuata makubaliano yaliyofikiwa ya mkataba wao. Kwa sababu Ndowo aliajiriwa kazi sehemu ya mapokezi (Receptionist) na wakati akiwa kazini alipelekwa mafunzo ya Telephone Operator/Receptionist na kupata vyeti, hivyo kwa mfanyakazi bora uajiri ungemhamishia kwenye nafasi ya Telephone Operator nafasi ambayo walimwajiri Margreth Chagula badala ya kumpunguza kazi mlalamikaji. Hii inaonyesha wazi kuwa walikiuka makubaliano ya mkataba. Vile vile hakuna ubishi hata kwenye maelekezo yake mwajiri alikubali kumwajiri Telephone Operator. Kwa hakika uajiri ulikuwa hauna sababu ya kumpunguza mfanyakazi huyu licha ya kampuni kuwa na sababu zao za kiuchumi ndani ya kiwanda hicho.

Tukirudi nyuma Bi. Ndowo hakuwahi kupewa onyo lolote la utendaji wake wa kazi kama ni hivyo mahakama haikuwahi kuelezwa hivyo juu ya tabia mbaya ya mdai huyu.

Hivyo basi kupunguzwa kazi kwake siyo halali. Ingawa mshauri Mr. Pazi anaona ni vema kumrejsha kazini, mimi naona kuwa itakuwa si vema kumrejsha kazini kwani toka Mei, 1998 alipopunguzwa kazi ni miaka mitatu (3) na si vema kuamuru arejeshwe kazini kwa vile atalipwa kwa kazi ambayo hakumfanyia mwajiri. Kwa maoni yangu naamuru mwajiri amlipe fidia ya miezi (18) kumi na nane kwa kupoteza ajira.

Kuhusu malipo ya posho ya kujikimu nakubaliana na Bw. Pazi haiwezekani kwa vile mwajiri alishamlipa mafao yake yote.

Uamuzi huu umesomwa leo tarehe 25/7/2001 mbele ya Mlalamikaji na unakuwa TUZO ya Mahakama ya Kazi.

(Sgd)

C. E. R. WILLIAM
Naibu Mwenyekiti
25/7/2001

Certified true copy of the original

1 Agosti, 2001

B. E. NYAMUBI,
Registrar

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 130

MAOMBI YA MAREJEO NA. 13 MWAKA 1999 9
(Katika Mahakama ya Kazi ya Tanzania, Dar es Salaam)

baina ya

TANGANYIKA PACKERS LTD., DAR ES SALAAM
na

PETER M. ITINDE, DAR ES SALAAM

SHAYO, D/C;

Haya ni maombi ya marejesho ya kupinga uamuzi uliotolewa na Mh. Mlelwa, Naibu Mwenyekiti (kama alivyokuwa) katika shauri la uchunguzi wa Mgogoro wa

Kikazi Na. 54/97 baina ya Peter M. Itinde na Tanganyika Packers Ltd., Dar es Salaam. katika shauri hilo mlalamikiwa Tanganyika Packers Ltd., ambaye alikuwa anawakilishwa na Wakili msomi Bw. Kariwa, alitoa pingamizi la awali kuwa shauri hilo halikuwepo Mahakamani kihalali kwa vile lililetwa nje ya muda uliowekwa kisheria, hivyo kuifanya Mahakama hii ya kimwanzo kutokuwa na mamlaka/uwezo kisheria kuchunguza mgogoro huo. Ilielezwa mbele ya mahakama hii ya kimwanzo, na mlalamikaji, Peter Itinde hakuwa na ubishi, kuwa mlalamikaji alikuwa amefukuzwa kazi tarehe 30/4/91 na alifikisha malalamiko yake kwa Kamishna wa Kazi tarehe 23/4/97 naye Kamishna wa Kazi aliwasilisha mgogoro huu wa uchunguzi Mahakamani tarehe 14/8/97. Kwa hali hiyo muda ulishapita kwa miaka saba na miezi minne tangia ufukuzwe kazi mpaka mgogoro kufikishwa Mahakamani, kinyume na Sheria ya Ukombo wa Muda (Law of Limitation Act 1971) jedwali la kwanza, ibara ya saba. Akitoa Uamuzi wake, Mh. Mlelwa (DC) alisema kuwa mlalamikaji alifikisha lamamiko lake kwa Kamishna wa Kazi ndani ya miaka sita (30/4/91 — 23/4/97), na kama Kamishna wa Kazi hakupeleka Mahakamani mgogoro huo muda unaotakiwa, hilo siyo kosa la mlalamikaji. Kwa hivyo pingamizi la awali la mlalamikiwa likatupiliwa mbali.

Akiwa hakuridhishwa na Uamuzi huo, msomi Kariwa kwa niaba ya muomba marejeo — Tanganyika Packers Ltd., Dar es Salaam ameleta maombi ya marejeo ya uamuzi huo dhidi ya majibu marejeo Peter Itinde. Katika tamko lake la marejeo (statement of revision) msomi Kariwa ametoa sababu nne, nazo ni zifuatazo:—

1. That the learned Deputy Chairman erred in law and fact for failing to decide the matter before him basing on the facts as pleaded by the respondent in the complaint (kumbukumbu za madai) and for resorting into other extraneous sources of information not disclosed to the Applicant thus denying the applicant the right to contest the validity of the sources and the contents thereof.
2. The learned Deputy Chairman erred in law far advocating for Respondent's cause without being invited by any party thus failing to act impartially.
3. The learned Deputy Chairman erred in law and facts for holding that the limitation time to file a dispute in the Industrial Court of Tanzania ceases to run once a complaint is lodged with the commissioner for Labour no matter how long it takes the Commissioner to report the dispute in the Industrial Court.
4. The learned Deputy Chairman erred in facts and law in failing to hold that the Dispute was filed in Court after the limitation of time had expired and the Respondent was even time barred at the time the complaint was lodged with the Commissioner for Labour

Mjibu marejeo alipelekwa substituted service kwenye Gazeti la Majira. Alitoa nakala ya gazeti hilo la tarehe 1/7/

2001 kama kielelezo R 1, na pia risiti ya kutangaza kwenye gazeti hilo — kielelezo R 2 ya tarehe 1/7/2001. Baada ya kuridhika na maelezo hayo, Mahakama hii ya Marejeo ilikubali kusikiliza marejeo haya upande mmoja — exparte kwa vile mjibu marejeo alipelekwa taarifa kwenye gazeti na hakumudu kufika kujitetea kwenye marejeo haya.

Katika kutoa maelezo yake, Msomi Ngudungi aliamua kuachana na hoja ya kwanza na ya pili na kuzungumzia kwa pamoja hoja ya tatu na ya nne ya sababu zake za marejeo. Alisema kuwa Uamuzi wa Mh. Mlelwa (DC) haukuwa sahihi kwani ulikwenda kinyume na matakwa ya Sheria. Akifafanua alisema Uamuzi ulisema kuwa mjibu marejeo alifukuzwa kazi tarehe 30/4/91 na akapeleka taarifa kwa Katibu wa Juwata tarehe 15/5/91, na kwamba sio kweli alifukuzwa kazi tarehe 30/4/90. Kwa hiyo, alisema Mh. Mlelwa tokea tarehe 30/4/97 lalamiko lilipelekwa kwa Kamishna wa Kazi ni miaka mitano na siku 23, ndani ya muda wa miaka sita.

Msomi Ngudungi anadai kuwa msimamo huo wa Mh. Mlelwa (DC) ni kinyume na taratibu za kisheria kuhesabu muda tangu lalamiko lifikishwe kwa Kamishna wa Kazi. Anaendelea kusema kwa kishindo kuwa mjibu marejeo alifukuzwa kazi tarehe 30/4/91 na kwa mtazamo wa Mh. Mlelwa (DC) kipindi cha kuchukua hatua (cause of action) kitaanza pale alipopeleka kwa Kamishna wa Kazi. Lakini anasema, barua ya Kamishna kuleta mgogoro Mahakama ya Kazi ni tarehe 14/8/97, ndiyo kusema Mahakama hii ya kimwanzo ilisikiliza shauri baada ya miaka 6 na miezi 4 kinyume na Sheria ya Ukomo wa muda ambao ni miaka 6 kwa mikataba ya ajira, na kwamba muda unatakiwa kuhesabiwa tangu pale Kamishna wa Kazi alipofikisha mgogoro Mahakamani. Aliitaka mahakama hii ya marejeo kurejea maamuzi katika *Uchunguzi wa Mgogoro wa Kikazi Na. 20/2000 kati ya Wafanyakazi 184 wa A.T.C. Vs A.T.C. na Misc. CC 14/94 N.M.C. Vs Hamisi Juma & Others* (zote hazijaripotiwa), ambazo zilisitiza kuwa lazima Mgogoro wa Uchunguzi ufikishwe Mahakama ya kazi ndani ya miaka 6 kwa mujibu wa Sheria ya Ukomo wa muda 1971, maana ni madai yanayotokana na mikataba ya ajira. Kwa hivyo basi, Msomi Ngudungi anatoa rai kuwa maombi ya marejeo yakubaliwe na mahakama hii ya marejeo.

Tumepata fursa ya kupitia kwa kina mwenendo na uamuzi wa Mahakama hii ya kimwanzo (Mh. Mlelwa (DC) katika Uchunguzi wa Mgogoro wa Kikazi Na. 54/97, na pia tamko/kumbukumbu la marejeo na maelezo ya Msomi Kariwa akishikiliwa mkoba na msomi Ngudungi, kwa niaba ya muomba marejeo — Tanganyika Packers Ltd. Kwa pamoja na kwa kauli moja, Jopo zima la marejeo tumeridhika kuwa kulingana na kumbukumbu na maelezo yaliyotolewa mbele ya Mahakama hii ya kimwanzo kwenye pingamizi la awali, ni ukweli ulio wazi na usioweza kupingika kwamba mjibu marejeo alifukuzwa kazi tarehe 30/4/91 na ndipo kisheria chanzo cha kuchukua hatua (cause of action) kilianza. Ni ukweli pia kwamba mjibu marejeo alipeleka lalamiko lake kwenye mamlaka inayohusika — Kamishna wa Kazi, tarehe 23/4/97. Baada ya Kamishna wa Kazi kulifanyia kazi lalamiko hilo, alibaini kuwa kuna mgogoro unaofaa

kufanyiwa uchunguzi na Mahakama ya kazi, kwa hiyo akauleta kwa Mwenyekiti wa mahakama ya kazi tarehe 14/8/97 takriban baada ya miezi minne tangu alipopokea lalamiko toka kwa mjibu marejeo.

Ni ukweli pia kwamba, migogoro ya uchunguzi ni ya aina ya madai yanayoangukia kwenye mkondo wa mikataba, yenyewe yakiwa yametokana na mikataba ya ajira. Chini ya Sheria ya ukomo wa muda (Law of Limitation Act 71) jedwali la kwanza aya ya 7, ukomo wa muda wa kufungua madai yatokanayo na mikataba ni miaka sita. Kama huo ndio msimamo wa kisheria, ndiyo kusema basi Kamishna wa Kazi alipouleta mgogoro Mahakamani kwa uchunguzi tarehe 14/8/97, ndiyo tarehe muafaka ya kuanza kupima muda wa mgogoro kama uko ndani ya miaka 6, na sio tarehe 23/4/97 siku ambapo mjibu marejeo alipofikisha lalamiko lake kwa Kamishna wa Kazi kama alivyoamua Mh. Mlelwa (DC), jambo ambalo tunadhani alipotoka kisheria. Kwa hesabu za karibu basi, tukianza tarehe hiyo 14/8/97 mpaka tarehe 30/4/91 siku ambayo mjibu marejeo alifukuzwa kazi, tunapata miaka 7 na miezi 3½. Ndiyo kusema, kama msomi Ngudungi anavyodai, uchunguzi wa mgogoro huo ulipoletwa Mahakamani tayari ulishapitwa na wakati (time barred), na hivyo kuufanya usiwepo mbele ya mahakama hii ya kimwanzo kihalali.

Hata hivyo, ni vema tukaliweka wazi kuwa, chanzo cha ucheleweshaji huo kinatokana hasa na mjibu marejeo mwenyewe. Alilalia haki yake ya kudai tangu tarehe 30/4/91 alipofukuzwa kazi hadi tarehe 23/4/97 alipoamka usingizini na kukimbilia kwa Kamishna wa Kazi kulalamika. Tunadhani hata tarehe hiyo 23/4/97 alipopeleka barua ya malalamiko kwa Kamishna wa Kazi, tayari muda ulishapita wa Kamishna kuleta shauri Mahakamani, maana kama hatua zingechukuliwa mapema, basi Kamishna wa Kazi alipashwa awe ameleta mgogoro Mahakamani kwa Uchunguzi siyo baada ya tarehe 29/4/96. Kwa hiyo mjibu marejeo hana budi kujilaumu kwa kulalia haki yake muda wote huo, hata kusababisha Kamishna wa Kazi kuleta mgogoro Mahakamani ukiwa tayari nje ya muda. Kama Mh. Mlelwa (DC) angejielekeza vema juu ya hali hiyo, bila shaka asingelikia uamuzi huo wa makosa kuwa mlalamikaji/mjibu marejeo alifikisha lalamiko lake kwa Kamishna wa Kazi ndani ya miaka sita, na kama Kamishna huyo hakupeleka mahakamani shauri hilo kwa muda unaotakiwa, hilo sio kosa la mlalamikaji.

Kama tulivyobainisha hapo juu, kisheria mwenye mamlaka ya kufungua migogoro ya uchunguzi wa kikazi Mahakama ya Kazi ni Kamishna wa Kazi peke yake na si mtu mwingine yeyote. Hiyo ni kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama ya Kazi Na. 41/67 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 3/90 na Na. 2/93. Na Kamishna wa Kazi huwa anafungua mgogoro kwa uchunguzi Mahakama ya Kazi, baada ya kupokea lalamiko la mwathirika na kulifanyia kazi na kisha kuridhika kuwa kuna mgogoro unafaa kufanyiwa uchunguzi na Mahakama ya Kazi, kama alivyofanya katika Shauri hili. Sasa kwa vile Kamishna alipopokea lalamiko la mjibu marejeo hiyo tarehe 23/4/97, na tayari muda wa miaka

sita ulishapita, tunadhani asingeliweza kukataa kulileta Mahakama ya Kazi kwa vile yeye ni mtawala tu na hana uwezo wa kimahakama wa kusema suala hilo liko nje ya muda. Jukumu lake kama mtawala lilikuwa kullishughulikia lalamiko hilo na kisha kulifikisha mbele ya mahakama ya Kazi kwa uchunguzi na uamuzi. Kwa hivyo basi, ilikuwa ni jukumu la mahakama hii ya kimwanzo kuona kwamba kilichokuwa kimeletwa Mahakamani kwa uchunguzi kilikuwa ndani ya muda halali au hapana.

Kwa vile basi Mahakama hii ya kimwanzo ilipotoka kisheria katika kuona uhalali wa Mgogoro wa Uchunguzi kutokana na wenyewe kuwa nje ya muda, sawa na pingamizi la awali la muomba marejeo, Mahakama hii ya Marejeo haina budi kutamka kuwa Mgogoro wa Uchunguzi Na. 54/97 ulikuwa umeletwa nje ya muda kama tulivyoelezea hapo juu, na hivyo haukuwa mbele ya Mahakama hii ya kimwanzo kihalali. Kwa hitimisho basi, tunatengua na kuweka kando uamuzi wa Mhe. Mlelwa Naibu, Mwenyekiti (Kama alivyokuwa), na tunaamua kuwa Mgogoro wa Uchunguzi Na. 54/97 utupiliwe mbali kama ulivyoletwa.

Uamuzi huu unakuwa TUZO ya Mahakama ya Kazi na unakuwa na nguvu ya kisheria mara moja.

Umetolewa nasi leo hii tarehe 26 mwezi wa saba mwaka 2001 mbele ya wahusika.

(sgd)

E. L. K. MWIPOPO, J.
Mwenyekiti

(sgd)

A. A. M. Shayo
Naibu Mwenyekiti

(sgd)

C. E. R. WILLIAM
Naibu Mwenyekiti

Certified true copy of the original

8 Agosti, 2001

B. E. NYAMUBI,
Registrar

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 131

UTHIBITISHO NA USIMAMIAJI WA MIRATHI

(Katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam)

SHAURI NAMBARI 74 YA MWAKA 2001

Uthibitisho na Usimamiaji wa Mirathi ya
Rajabul Nasser Shariff, Marehemu
na

Shamshudin Jaffer, Mwombaji

TAARIFA YA KAWAIDA (Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamiaji wa Mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 20 mwezi wa 6 mwaka wa 2002.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 20 mwezi wa 3 mwaka 2002.

.....
Naibu Msajili Mwandamizi